

CHANJO YA COVID-19

KILE CHA KUTARAJIA


Huna uhakika wa kile cha kutarajia wakati wa kupokea chanjo ya COVID-19?
Kuwa tayari – pata kujua ukweli!



DOZI MBILI, KILA BAADA YA WIKI 3 – 4.

Inahitajika kuchukua dozi zote mbili, kwani chanjo haitakuwa na ufanisi ikiwa utapokea dozi moja tu.

Ni muhimu kupata chanjo ya aina ileile kama dozi ya kwanza.



USUMBUFU WA MUDA MFUPI UNAWEZEKANA.

Uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, baridi, homa ya joto na maumivu kwenye eneo lililodungwa sindano yameripotiwa. Athari hizi kali ni za kawaida, hutokea na zinatarajiwa. Utendakazi mbaya wa mwili hauwezi kutokea. Madhara haya kawaida hudumu saa 24-48 na kawaida huwa makubwa zaidi baada ya dozi ya pili. Athari ni **JAMBO NZURI** – inamaanisha mwili unafanya kazi yake na kuunda kingamwili.



ULINZI HUTOKEA WIKI 1 – 2 BAADA YA DOZI YA PILI.

Muda ule chanjo itatoa kinga utapata kujulikana kadri muda unavyopita na utafiti unavyofanywa.



MASKI, KUWEKA UMBALI KATI YAKO NA WENGINE NA UPIMAJI ZINABAKIA KUWA MUHIMU.

Sawa na chanjo zingine, watu kadhaa watahitaji kupatiwa chanjo kabla ya maambukizi kushuka kwa kiwango kinachorudisha maski na vizuizi vingine.



Jefferson Health®

HOME OF SIDNEY KIMMEL MEDICAL COLLEGE

HADITHI

SITA ZA UWONGO KUHUSU COVID-19

ZIMEFUNULIWA

Wacha tuweke rekodi kamili kuhusu hadithi za uwongo kuhusiana na chanjo ya COVID-19.



HADITHI YA UWONGO: CHANJO YA COVID-19 SI SALAMA KWA SABABU ILITENGENEZWA NA KUJARIBIWA KWA HARAKA.

Ukweli: Kampuni nyingi za dawa zimewekeza rasilimali muhimu katika kukuza haraka chanjo ya COVID-19 kwa sababu ya athari ya janga ulimwenguni. Hii ilipelekea mkalibiano wa dharura, lakini hiyo haimaanishi kampuni hazikuwa salama au hazikufanya upimaji wa kutosha. Wakati mwingu uliokolewa wakati wa mchakato wa uandalizi/ukaguzi.



HADITHI YA UWONGO: TAYARI NILIKUWA NA COVID-19 NA NIKAPONA, KWA HIVYO SIHITAJI KUPATA CHANJO YA COVID-19.

Ukweli: Hakuna habari ya kutosha kwa sasa kusema ikiwa au kwa muda gani baada ya kuambukizwa mtu analindwa kutokana na kuambukizwa COVID-19 tena. Unapaswa kupata chanjo ya COVID-19, hata ikiwa umewahi kuwa na COVID-19 hapo awali. Hata hivyo, wale ambao wamekuwa na COVID-19 wanapaswa kuchlewesha chanjo hadi siku 90 baada ya utambuzi.



HADITHI YA UWONGO: KUNA ATHARI KALI KUTOKANA NA CHANJO ZA COVID-19.

Ukweli: Katika hali nadra watu wengine wamekuwa na athari ya mzio muda mfupi baada ya chanjo. Vinginevyo, athari inayojulikana ya chanjo ni ya muda mfupi na nyepesi au wastani. Watu wengine wanaweza kupata maumivu ya kichwa, baridi, uchovu au maumivu ya misuli au homa ya joto inayodumu kwa siku moja au mbili. Kumbuka kwamba athari hizi mara nyingi humaanisha kuwa mwili wako unaitikia chanjo.



HADITHI YA UWONGO: SITAHITAJI KUVAA MASKI BAADA YA KUPATA CHANJO YA COVID-19.

Ukweli: Inaweza kuchukua muda kwa kila mtu ambaye anataka chanjo ya COVID-19 kupata moja. Na ingawa chanjo inaweza kukuza usiugue, haijulikani kwa wakati huu ikiwa bado unaweza kueneza virusi kwa wengine. Hadi tujue zaidi, kuvala maski na kukaa futi sita mbali na wengine itakuwa muhimu.



HADITHI YA UWONGO: NINAWEZA KUAMBUKIZWA COVID-19 KUTOKANA NA CHANJO.

Ukweli: Huwezi kuambukizwa COVID-19 kwani chanjo hazina virusi vilivyo hai.



HADITHI YA UWONGO: NINA SHIDA ZA KIAFYA KWA HIVYO SIWEZI KUPEWA CHANJO.

Ukweli: Ndiyo, unaweza kupokea chanjo. Kwa kweli, watu walio na shida za kiafya, kama shinikizo la damu, ugonjwa wa kisukari na magonjwa ya moyo wanapaswa kupewa chanjo. COVID-19 inaweza kuwa mbaya zaidi kwa watu walio na hali hizi.



Jefferson Health®

HOME OF SIDNEY KIMMEL MEDICAL COLLEGE

Hakimiliki © 2021 Jefferson Health. Haki zote zimehifadhiwa. Yaliyomo kwenye hati hii hayakusudiwi kutumika kama ushauri wa kimatibabu, lakini yanatolewa kama huduma ya afya ya umma kulingana na maeleo kutoka kwa vyando vinavyopatikana kwa umma, ikijumuisha Vituo vya Udhibiti wa Magonjwa, Utolewaji wa Chakula na Dawa na mamlaka zingine. Tafadhal wasiliana na mtaalamu wa kimatibabu kwa maswali ya ziada kuhusu COVID-19 au chanjo, au ikiwa unaufikiria unaweza kuwa na COVID-19.